AGCOT
AGRICULTURAL GROWTH CORRIDORS OF TANZANIA

*Championing sustainable food systems*

NEWS & FEATURES

# Tanzania Mpya, Dira Mpya: Toa Maoni Yako Kwenye Dira ya Maendeleo 2050!

**Published: 20 December 2024**

**Wadau wa SAGCOT, wanufaika, na washirika wote, mnakaribishwa kushiriki katika kongamano muhimu la mtandaoni kujadili Rasimu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.**

---

📅 **Tarehe:** Jumatatu, 23 Desemba 2024
⏰ **Muda:** Saa 4:00 asubuhi – 6:00 mchana
📍 **Mahali:** Mtandaoni kupitia Microsoft Teams

---

## Rasimu ya Dira ya Maendeleo 2050

Rasimu hii, iliyozinduliwa na **Rais wa Zanzibar, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, inalenga kuweka msingi wa maendeleo endelevu ya Tanzania kuelekea mwaka 2050.

Kwa sasa, Dira imeingia katika **awamu ya uhakiki**, ambapo maoni ya wadau kutoka sekta mbalimbali ni muhimu kuhakikisha inaakisi mahitaji na ndoto za Watanzania wote.

## Hatua Zinazofuata

🔹 **Ushirikishwaji wa Wadau:** Desemba 2024 – Januari 2025
Kama alivyoeleza **Mhe. Prof. Kitila Mkumbo**, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji,, kipindi hiki ni fursa ya pekee kwa wadau kutoa maoni yao na kushiriki katika kujenga Tanzania mpya.

---

## Kwa Nini Kushiriki ni Muhimu?

Huu ni wakati wako wa:

- Kuchangia maoni katika mustakabali wa **kilimo, uchumi**, na maendeleo ya kijamii.
- Kuimarisha ushirikiano kati ya wadau wa kilimo na maendeleo ya kitaifa.
- Kusaidia kuhakikisha Dira hii inaleta matokeo chanya kwa kila Mtanzania.

---

👉 **Jiunge Sasa:** Bonyeza Hapa
Au tumia **QR Code** iliyopo kwenye bango la tangazo.

---

**Usikose! Toa Maoni Yako Leo. Pamoja Tunaweza Kujenga Tanzania Mpya.**

Published 20 December 2024 · News & Features

Source: https://agcot.org/2024/12/20/tanzania-mpya-dira-mpya-toa-maoni-yako-kwenye-dira-ya-maendeleo-2050/ · AGCOT Centre, Dar es Salaam